OFISI YA RAIS – TAMISEMI
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE

SHULE YA SEKONDARI SAJA,
S.L.P 90,
MAKAMBAKO

KUMB. NA. SSS/K.1/2021
JINA LA MWANAFUNZI……..
SHULE YA MSINGI …….
S.L.P……
MAKAMBAKO.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SAJA KIDATO CHA KWANZA 2021

Napenda kukupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Saja mwaka 2021. Nafasi uliopewa inaliliwa na wengi hapa nchini kwa waliokosa. Hivyo huna budi kuijali, kuitumia kwa manufaa yako na Taifa kwa ujumla.

Shule hii ni ya mchanganyiko, ipo katika kata ya SAJA, ipo umbali wa kilomita 18 toka mjini Makambako. Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021.

KARIBU SANA SAJA SEKONDARI

……..
KOMBA F.A
(MKUU WA SHULE)
(0762 852 112)

ZINGATIA MAELEKEZO

MAMBO YA KUZINGATIA

(a) **SARE ZA SHULE**

Shule hii ina sare mbili (2) kwa wavulana na wasichana.

(i) WASICHANA

- Blauzi (02) nyeupe (nusu kanzu) zenye mikono mirefu, shingo ya duara na ziwe na urefu wa kupita kwenye magoti.
- Suruali mbili (02) rangi ya damu ya mzee na kijani mgomba (Angalia sampuli ya vitambaa)
- Viatu vya ngozi vyeusi visivyo na visigino virefu vya kufunga na kamba.
- Soksi nyeupe ndefu
- Sweta rangi ya bluu yenye shingo ya "V"
- Tai mbili ya rangi ya suruali
- Nguo za ndani zisizoungua kumi na mbili (12)
- Aje na picha (passport size) moja ya rangi
- Aje na vifaa vya usafi (Fagio la chelewa moja na Jembe moja)

(ii) WAVULANA

- Mashati mawili (02) meupe (Tetroni mikono mifupi)
- Suruali mbili (02) za heshima rangi ya damu ya mzee na khaki kitambaa kizito (Angalia sampuli ya vitambaa)
- Sweta rangi ya bluu yenye shingo ya "V"
- Tai mbili (02) ya rangi ya suruali
- Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na visigino virefu vya kufunga na kamba
- Soksi nyeusi ndefu.
- Nguo za ndani zisizopungua sita (06)
- Aje na picha (passport size) moja ya rangi
- Aje na vifaa vya usafi (Fagio la chelewa moja na Jembe moja)

(b) **SARE ZA MICHEZO**

(WASICHANA NA WAVULANA)

- Tracksuit nyeusi zenye miraba meupe
- Raba nyeusi jozi mbili (02)

(c) **VIFAA VYA MASOMO**

- Daftari kubwa za kutosha (counter books) 10 (2 quire)
- Mkebe na vifaa vyake
- Aje na English to English dictionary pamoja na kamusi ya Kiswahili
- Aje na begi kubwa kwa ajili ya kubebea daftari zake
- Aje na faili moja (01) kwa ajili ya kutunzia mitihani yake
- Kiti na meza kwa anaye hamia au pesa (40,000/=)

(d) **MAHITAJI YA CHAKULA**

- Aje na mahindi debe kumi (10) kwa mwaka
- Aje na maharage debe tatu (03) kwa mwaka
- Aje na mchele debe moja (01) kwa mwaka

ZINGATIA MAELEKEZO

- Aje na sahani, kikombe, na kijiko
- Aje na ndoo ndogo moja
- Sukari kilo nne (4) kwa mwaka kwa anayekaa hosteli
- Aje na fedha shilingi laki moja (100,000/=) kwa ajili ya kuandaa chakula hicho, yaani kusaga na kukoboa, pamoja na kununua mafuta, chumvi viungo n.k (KWA MWAKA)

MAHITAJI YA HOSTELI

- Gauni mbili rangi ya pinki yenye mshono wa soro (kitambaa cha koshibo) kwa wasichana
- Tisheti mbili rangi ya njano ambazo hazina maamndishi wala michoro na picha (kwa wavulana)
- Suruali mbili nyeusi mshono wa kawaida (suruali za jinzi hazihitajiki - kwa wavulana)
- Shuka mbili rangi ya bluu bahari na pinki kwa wasichana na wavulana
- Aje na godoro mita mbili na nusu na chandarua ya kuzuia mbu (kwa wote)
- Aje na sanduku la bati lenye kufuli kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake. (kwa wote)
- Aje na sweta la kijani kwa ajili ya kushindia wakati wa baridi.
- Aje na Tochi kwa matumizi ya usiku
- Aje na bunda moja la karatasi (RIMU) kwa matumizi yake binafsi

MUHIMU

- Nimarufuku kwa mwanafunzi kuja na nguo za nyumbani. Wanafunzi wote wataishi hosteli.
- Wanafunzi wote wanatakiwa kula shuleni
- Unaweza lipia michango hiyo kwa awamu nne (04) (kwa miezi mitatu mitatu).
- Kabla ya kuja shuleni jaza fomu zifuatazo na uje nazo siku ya kuripoti
  (a) Fomu ya kukubali nafasi ya kujiunga kidato cha kwanza
  (b) Fomu ya maelezo binafsi ya mwanafunzi
  (c) Fomu ya kupimwa afya yako (medical examination form). **Pima katika hospitali za serikali tu.**

NB: *Fedha zote zitapokelewa ofisi ya uhasibu na si vinginevyo*

HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE

SHULE YA SEKONDARI SAJA,

S. L. P 90 MAKAMBAKO.

MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

A. TAARIFA YA MWANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi_____
2. Tarehe ya kuzaliwa _____
3. Mahali alipozaliwa. Wilaya_____Mkoa_____
4. Dini_____ Dhehebu_____

B. TAARIFA ZA WAZAZI

1. Baba yu hai? Ndio/Hapana_____
2. Mama yu hai? Ndio/Hapana_____
3. Jina la mzazi/Mlezi anayekulea_____
4. Uhusiano wako na mlezi (kama huna wazazi)_____
5. Kazi ya mzazi/Mlezi_____
6. Anuani ya mzazi/Mlezi_____
7. Namba za simu za mzazi/Mlezi_____
8. Mahali aishipo mzazi/mlezi: Kijiji/Mji_____ Kata_____
   Tarafa _____ Wilaya_____ Mkoa_____

C. NDUGU WENGINE WA KARIBU

1. Ndugu_____
   Anuani_____
   Uhusiano na mwanafunzi_____

2. Ndugu_____
   Anuani_____
   Uhusiano na mwanafunzi_____

D. UTHIBITISHO WA AFISA MTENDAJI WA KATA AU MWENYEKITI WA KIJIJI AU WA KITONGOJI AMBAKO MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI ANAISHI

1. Jina la kiongozi_____

   Anuani_____ saini na muhuri_____

2. Jina la kiongozi_____

   Anuani_____ saini na muhuri_____

ZINGATIA MAELEKEZO

HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE

SHULE YA SEKONDARI SAJA,

S. L. P 90 MAKAMBAKO.

FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SAJA SEKONDARI 2021

SEHEMU A: (IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE)

Mimi_____ (Jina la mwanafunzi) nimesoma na kuelewa masharti yote na sheria za shule. Nayakubali*/Siyakubali. Naipokea/Siipokei nafasi hii niliyopewa. Ninaahidi kuwa nitazingatia masharti na sheria zote za shule na nitakua mtiifu mpaka nitakapomaliza kidato cha nne

Saini ya mwanafunzi_____ Tarehe_____

SEHEMU B: (IJAZWE NA MZAZI/MLEZI)

Mimi_____ mzazi/mlezi wa_____
Ninakubali*/Sikubali nafasi aliopewa mtoto wangu. Ninaahidi kumtimizia mahitaji yote ya shule na kusaidiana na walimu kumlea mtoto huyu kimwili, kiakili na kiroho mpaka atakapohitimu masomo yake.

Saini ya mzazi/mlezi_____ Tarehe_____

***futa isiyohusika**

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Sheria za shule zinalenga katika kumlea mwanfunzi awe na nidhamu, azingatie maadili ya Taifa letu na hatimaye aishi kama raia mwema anayekubalika katika jamii yetu.
Ni imani yetu kuwa shule yenye wanafunzi wenye nidhamu hufanya vizuri katika taaluma.

HIVYO NI LAZIMA KWA KILA MWANAFUNZI WA SHULE HII

1. Kuhudhuria masomo kila siku, tatizo la ugonjwa, msiba n.k litaombewa ruhusa.
2. Kusalimu watu wote na hasa waliomzidi umri
3. Kusimama mwalimu anapoingia darasani na wakati wa kuuliza na kujibu swali
4. Kuwahi shuleni na kufanya usafi katika eneo alilopangiwa
5. Kuvaa nguo za heshima ndefu shuleni na hata nyumbani
6. Kutii sheria zote za shule
7. Ni muhimu kutunza usafi wako binafsi na mazingira ya shule
8. Kukaa kimya kwa nidhamu darasani
9. Usizungumze na mwalimu au mtu aliekuzidi umri ukiwa umekaa, mikono ikiwa mfukoni ama kofia kichwani au ukiwa umevaa miwani ya jua
10. Mwanafunzi haruhusiwi kutembea usiku bila sababu yoyote hata kama atakua kwa wazazi wake
11. Mwanafunzi asiruhusiwe kufanya sherehe za usiku
12. Daima uwe msafi kimwili na mavazi. Uwe na nywele fupi, nywele ndefu au masharubu haviruhusiwi shuleni
13. Ni marufuku mwanafunzi kujiunga na vilabu vya michezo nje ya shule
14. Ni marufuku mwanafunzi kushiriki katika vigenge vya usengenyaji au kusema uongo
15. Usifanye biashara aina yoyote shuleni
16. Usichelewe siku za kufungua shule au usiongeze siku za ruhusa
17. Usikatae uteuzi wa kushiriki katika shughuli za michezo n.k
18. Usigune wakati mwalimu au kiongozi yeyote anapotoa tangazo, kama kuna swali nyosha mkono utaratibu ufuatwe
19. Usibandike au kuandika tangazo lolote lile bila ruhusa ya mwalimu anayehusika

“MAISHA YA SHULE NI MAZURI KWA WALE TU WATAKAOFUATA SHERIA ZA SHULE”

ZINGATIA MAELEKEZO

NI MARUFUKU KWA MWANAFUNZI

(a) Kutumia lugha chafu kama matusi n.k
(b) Kutembelea nyumba za kulala wageni au za kulala walimu, baa, vilabu vya pombe na kumbi za starehe
(c) Kufuga kucha, nywele, ndevu, kuvaa mikufu, kupaka marashi au rangi kwenye kucha au kuvaa hereni, kuwa na redio, kamera, simu za mkononi awapo shuleni
(d) Kufanya mapenzi na wanafunzi wenzake au na watu wengine nje na ndani ya shule
(e) Kuambatana na makundi ya wahuni wa mtaani
(f) Kuondoka shuleni kabla ya mda wa masomo kuisha (utoro)

MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI AFUKUZWE SHULE MARA MOJA

(a) Wizi
(b) Uasherati, ubakaji na ushoga
(c) Ulevi wa aina yoyote, pombe au madawa ya kulevya
(d) Uvutaji bangi
(e) Makosa ya jinai Kupigana au kupiga
(f) Kuoa au kuolewa
(g) Kupata mimba au ksababisha mimba ndani ya shule na nje ya shule
(h) Kutoa mimba au kitumia vidonge au njia za uzazi wa mpango
(i) Kuharibu kwa makusudi mali za umma Kudharau bendera au wimbo wa Taifa
(j) Kufanya, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au kuhatarisha amani ya shule wakati wowote ule
(k) Kukataa kutii amri ya mkuu wa shule au ya mwalimu yeyote.

MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECNOLOGY

SAJA SECONDARY SCHOOL,
P. O. BOX. 90,
MAKAMBAKO.
DATE……..

REF. NO. SSS/F.1/2021
THE MEDICAL OFFICER
…….
……

RE. REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Please kindly examine (name)……..to determine her/his physical and mental fitness for pursuing secondary school studies.

……
KOMBA F. A
(HEADMISTRESS)

1. Eyesight……
2. Hearing……
3. Speech……
4. Limbs……
5. Leprosy……
6. Epilepsy……
7. Cardiac disease……
8. Rheumatism……
9. Venereal disease……
10. Pregnancy (for girls)……
11. Any other serious disease……

I certify that the above named is fit/unfit to pursue his/her studies as required

Designation……..

Station……

Signature……

Date……

Stamp……..

ZINGATIA MAELEKEZO